

CHANJO

Pata chanjo zako ili uendelee kuwa na afya njema

Chanjo ni sindano unazodungwa ili uepoke kuwa mgonjwa


JE KWA NINI NINAHITAJI CHANJO?

Nchini Marekani, magonjwa mengi ambayo yaliwahi kuwafanya watu wawe wagonjwa zaidi yanatokomea. Mojawapo ya sababu kuu ya magonjwa haya kutokomea ni matumizi ya chanjo. Chanjo husaidia kuzuia magonjwa yanayoweza kusambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Ukidungwa sindano unazohitaji, unajikinga pamoja na wapendwa wako dhidi ya magonjwa.

CHANJO ZINAFANYA KAZI KIVIPI?

Chanjo inatengenezwa kutoka kwenye virusi vile vile (pia huitwa viini) vinavyosababisha ugonjwa. Viini vinavyotumika kutengeneza chanjo huwa "vimekufa" au dhaifu. Havitakufanya kuwa mgonjwa. Badala yake, vitasaidia mwili wako kupigana na viini na magonjwa yanayosababishwa na viini vile.

NI NANI ANAYEHITAJI CHANJO?



KUNAZO ATHARI ZA KANDO?

Watu wengine huwa na athari ndogo za kando baada ya kuchanjwa. Hizi zinapaswa kutoweka baada ya siku moja au mbili.




Maumivu/Wekundu

Upele Mdogo

Homa Ndogo

Watu wengine huwa na athari sugu za kando zisizo za kawaida, baada ya kuchanjwa. Mara nyingi, athari hizi hutokea dakika chache au saa chache baada ya kuchanjwa.



Tatizo la Kupumua

Kuhisi Kizunguzungu

Upele/Mwasho

Uvimbe wa Koo

NINAHITAJI CHANJO ZIPI?

Jedwali lililo upande ule mwingine linaonyesha chanjo ambazo watu wazima na watoto wanahitaji. Watu wazima ambao hawakupata chanjo zote walipokuwa watoto huenda wahitaji chanjo nyingi zaidi. Zungumza na daktari wako ili ujue ni chanjo zipi unazohitaji

Kwa maelezo zaidi, nenda kwenye: www.vaccines.gov

Jina la daktari wangu:

Nambari ya simu ya daktari wangu:

Pata chanjo zako ili uendelee kuwa na afya njema

Mwone daktari wako kwa ukaguzi wako na upate chanjo zozote mpya unazohitaji.

Chanjo zilizotiwa alama hapa chini zinahitajika kwa: _____
(Jina) _____ (Umri)

Ziara yako ijayo ni: _____ (asubuhi/mchana) _____
(Tarehe) _____ (Saa) _____ (Tarehe ya Kuzaliwa)

Chanjo unazohitaji	Inaitwaje?	Ni nani anayehitaji?			Chanjo ile inasaidia kukinga ugonjwa gani?	Ugonjwa ule unasababisha nini?
		Watoto* Pekee	Watoto na Watu Wazima	Watu Wazima Pekee		
<input type="checkbox"/>	DTaP au Td/Tdap		X		Dondakoo	Homa, uvimbe kooni na baridi
					Pepopunda	Maumivu ya misuli na wakati mgumu wa kupumua au kumeza
					Kifaduro	Kikohozi sugu na wakati mgumu wa kupumua, kula na kunywa
<input type="checkbox"/>	Mafua		X		Mafua	Maambukizi puani, kooni na mapafuni
<input type="checkbox"/>	HepA		X		Homa ya Manjano A	Aina ya ugonjwa wa ini
<input type="checkbox"/>	HepB		X		Homa ya Manjano B	Aina ya ugonjwa wa ini
<input type="checkbox"/>	Hib		X		Influenza ya haemofilasi aina ya b	Maambukizi ya tabaka la ndani karibu na ubongo na uti wa mgongo
<input type="checkbox"/>	HPV		X		Saratani ya kizazi	Aina ya saratani kwa wanawake
					Vifuro vya sehemu za siri	Aina ya ugonjwa unaoweza kusambazwa kwa kufanya ngono
<input type="checkbox"/>	IPV	X			Ugonjwa wa kupooza	Mwili kutoweza kusonga au wakati mwingine hata kupumua
<input type="checkbox"/>	MCV4		X		Homa ya uti wa mgongo	Maambukizi ya tabaka la ndani karibu na ubongo na uti wa mgongo
<input type="checkbox"/>	MMR		X		Ukambi	Homa, upele, mafua na kikohozi
					Matumbwitumbwi	Homa, maumivu ya kichwa na uvimbe wa sehemu ya mdomo inayotengeneza mate
					Surua	Homa, uvimbe wa tezi, na upele
<input type="checkbox"/>	PCV		X		Ugonjwa wa nimonia	Maambukizi ya mapafu
<input type="checkbox"/>	RV	X			Homa ya matumbo	Homa, kutapika na kuendesha
<input type="checkbox"/>	Varisela				Tetekuwanga	Upele wenye mwasho kote mwilini
<input type="checkbox"/>	Zosta			X	Vipele	Upele wenye maumivu makali na malengenge

* Watoto wa miaka 0 hadi 18

Jiweke na wapendwa wako salama kiafya. Pata chanjo zako.